

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA AWALI NA MAFUNZO YA UFUNDI
KIFURUSHI CHA MWEZI MEI -2020
KISWAHILI V

Muda; saa 2

JINA: _____ **MKONDO** _____ **TAREHE:** _____

MAELEKEZO

- Mtihani huu una sehemu A-E
- Jibu maswali yote kwa umakini
- Jibu lililofutwa au kukatwa halitosahihishwa
- Andika majina yako kwa herufi kubwa

SEHEMU A: MACHAGUO

Chagua jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu kwenye sehemu uliyopewa

1. Siku zote mwalimu anapoingia darasani hutuambia kuwa _____ kujifunza kwa bidii.
(a) Budi (c) Mawaidha
(b) Hatuna budi (d) Ni budi
2. Angela na Ritha wanapigiana mpira. Sentensi hii iko katika kauli ya _____
(a) Kutenda (d) Kutendea
(b) Kutendwa (e) Kutendeanana
(c) Kutendeka
3. Sisi ni wanafunzi wa darasa la tano. Neno sisi ni nafsi ya _____
(a) Pili wingi (d) Tatu umoja
(b) Kwanza wingi (e) Pili umoja
(c) Tatu wingi
4. Kinyume cha neno halali ni _____
(a) Halamu (d) Haramu
(b) Sana (e) Harari
(c) Alama
5. Jana Abeli alicheza mchezo mbaya sana. Neno lililopigiwa mstari limetumika kama _____
(a) Kitenzi (d) Kielezi
(b) Kivumishi (e) Kiwakilishi
(c) Jina (nomino)
6. Kuku jike anaitwa _____
(a) Koo (d) Kamba
(b) Jimbi (e) Kileo
(c) Kaa
7. Nilikuja hapa mara tatu. Maneno mara tatu ni _____
(a) Kitenzi (d) Kiunganishi
(b) Nomino (e) Kiwakilishi
(c) Kielezi

8. Rejina ni mtoto wa mjukuu wangu. Rejina ni _____
 (a) Mpwa wangu (d) Kilembwekeze
 (b) Kitukuu wangu (e) Kinying'inya
 (c) Kilembwe
9. Kinyume cha neno kashifu ni _____
 (a) Sifu (d) Hukumu
 (b) Aibisha (e) Kirimu
 (c) Karibisha
10. Ashura aliongeza bidii ya kazi atimaye akaishi vizuri. Methali ipi yenye maana sawa na sentensi hii? _____
 (a) Mchagua jembe si mkulima (d) Wingi si hoja
 (b) Elimu ni bahari (e) Mvumilivu hula mbivu
 (c) Jembe halimtupi mtu
11. "Tunacheza" katika neno hili kiambishi nafsi ni kipi? _____
 (a) -na - (d) - tu-
 (b) -ma- (e) Lima
 (c) -li -
12. Neno "paka" lipo katika ngeli ya _____
 (a) U -I (d) I-ZI
 (b) LI - YA (e) U-ZI
 (c) A-WA
13. Hali ya kuona haya baada ya kutenda au kufikiwa na jambo la fedheha huitwaje?
 (a) Tahayari (d) Tayari
 (b) Tashwishwi (e) Woga
 (c) Tathimini
14. Nomino inayotokana na "kuandika" ni _____
 (a) Mwandikieni (d) Kumwandikia
 (b) Mwandiko (e) Tumwandikie
 (c) Mwandika
15. Kauli taarifa ya sentensi isemayo "Nataka Asha ajibu swali hili upesi" _____
 (a) Jibu swali upesi Asha alitaka (d) Nataka ujibu swali hili upesi Asha
 (b) Jibu swali Asha upesi alitaka (e) Jibu swali upesi alitaka Asha
 (c) Alitaka Asha ajibu swali lile upesi
16. Andika neno ambalo halilandani na mengine. _____
 (a) Ninacheza (d) Ninaruka
 (b) Ninaimba (e) Ninalima
 (c) Ninakimbia
17. Kinyume cha neno LINGANISHA ni _____
 (a) Tafautisha (d) Fananisha
 (b) Potosha (e) Pangua
 (c) Rekebishia

18. Juma aliomba _____ yapunguzwe asishindwe kuoā.
 (a) Mandhari (d) Mahhali
 (b) Mahari (e) Maari
 (c) Maali
19. Kisawe cha neno “Faraghani” ni _____
 (a) Mafichoni (d) Kivulini
 (b) Pembezoni (e) Hadharani
 (c) Waziwazi
20. Alfajiri na mapema tuliondoka ukumbini. _____ mzizi katika neno hili”
 (a) –ndo- (d) –ondok-
 (b) -indoka (e) Doka
 (c) Ondoka
21. “urafiki wetu ni kama pete na kidole” maneno ambayo ni viunganishi ni _____
 (a) “kama na ni” (c) “wetu na pete”
 (b) “urafiki na wetu” (d) “pete na kidole
22. Neno la kiswahili lenye maana sawa na mwisho ni _____
 (a) Mwanzo (d) Utangulizi
 (b) Kifo (e) Pembezoni
 (c) Tamati
23. “Shule imefunguliwa” ukanushi wa sentensi hii ni upi? _____
 (a) Shule haitafunguliwa (d) Shule haikufunguliwa
 (b) Aujafunguliwa (e) Shule aikufunguliwa
 (c) Shule haujafunguliwa
24. Mtoto amechapwa fimbo na mama yake. Katika sentensi hii anayetenda jambo ni _____
 (a) Baba (d) Mtoto
 (b) Mama (e) Mtoto na fimbo
 (c) Fimob
25. Neno **SHAGHALABAGHALA** lina silabi ngapi? _____
 (a) Tano (d) Sita
 (b) Nane (e) Kumi na tano
 (c) Kumi na mbili
26. Ana alipigana kiume hadi mwisho. Kupigana kiume ni _____
 (a) Kama mwanaume (d) Bila woga
 (b) Bila silaha (e) Kama askari
 (c) Kwa woga
27. Maana ya kitendawili “Nimesafisha uwanja wangu kaja miguu mirefu kachafua” _____
 (a) Upepo (d) Mwanga
 (b) Mvua (e) Gari
 (c) Jua
28. Kijana huyu ana moyo mgumu. Kuwa na moyo mgumu ni kuwa na _____
 (a) Kiburi (d) Ukali
 (b) Kukomaa (e) Uvumilivu
 (c) Uhodari

29. Maana ya “kupiga chuku” ni _____
- (a) Kusema kwa mafumbo (d) Kusema kwa kwikwi
 (b) Kusema wazi wazi (e) Kusema kwa utani
 (c) Kusema uongo
30. “Chovya chovya umaliza buyu la asali” methali hii inafanana na _____
- (a) Haba na haba hujaza kibaba (d) Mgema akisifiwa tembo hulitia maji
 (b) Bandubandu huisha gogo (e) Mvumilivu hula mbivu
 (c) Cembe na chhembe mkate huwa

SEHEMU B: UFAHAMU

Soma habari ifuatayo kwa makini kisha jibu maswali

Wanangu nitakapokufa mimi, mtaitawala nchi hii. Wewe Mkwawa utakuwa Mtemi wa upande wa Kaskazini ya Iringa. Na wewe Muenga utakuwa Mtemi wa upande wa Kusini. Nawagawia hivyo ili kazi yenu iwe rahisi, jambo kubwa la muhimu la kukumbuka ni kudumisha ushirikiano, uhuru, heshima na umoja katika nchi ya wahehe. Msiposhirikiana kamwe kufanikiwa kazi yenu itakuwa ngumu. Mkwawa na Muhenga wakajibu kwa pamoja “Asante baba. Tutafanya kazi kama “ulivyotuagiza”

Maswali

31. Baba anatoa wosia kwa wanawe kuwa atakapokufa wao _____ wa nchi.
- (a) Watakuwa watawala (d) Wawakilishi
 (b) Viongozi (e) Raia
 (c) Wakazi
32. Mkwawa na Muhenga ni _____
- (a) Marafiki (d) Mapacha
 (b) Ndugu (e) Binadamu
 (c) Majirani
33. Kichwa cha habari ii kinafaa kwa methali isemayo _____
- (a) Samaki mkunje angali mbichi (d) Hakkuna marefu yasiyo na ncha
 (b) Dalili ya mvua ni mawingu (e) Kawia ufike
 (c) Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu
34. Habari hii inasisitiza _____
- (a) Kanuni bora za uongozi (d) Kuongoza kwa kujali maslahi
 (b) Utawala kwa demokrasia (e) Unaowaongoza
 (c) Kutawala kwa kunyenyekea
35. Mkwawa na Muhenga waliahidi _____ yale yote waliyohusiwa na baba yao,
- (a) Kutofuata (d) Kuitikia
 (b) Kutimiza (e) Kukataa
 (c) Kukumbuka

SEHEMU C: UTUNGAJI

Panga sentensi katika mtiririko mzuri kwa kuzipa herufi A-E

36. Nilipofika darasa la tano sikuamini kama ningemaliza shule ya msingi kwani masomo yalikuwa magumu.
37. Sasa naanza kufikiria jinsi ya kujiunga na elimu ya Sekondari
38. Nilipokuwa mdogo nilikuwa natamani sana nianza shule ili nijifunze mengi nisiyoyajua.
39. Lakini kama miujiza, sasa namaliza darasa la saba.
40. Ndoto yangu ikawa kweli pale mama aliponipeleka shule kuanza darasa la kwanza.

SEHEMU D: MATUMIZI YA LUGHA

Andika majina yafuatayo yako katika ngeli zipi

41. Panya _____
42. Mlango _____
43. Kigoda _____
44. Kochi _____
45. Chupa _____

SEHEMU E: BARUA

Jaza sehemu zilizoachwa wazi katika barua ifuatayo kwa kuchagua jibu sahihi kwenye kisanduku

Kata ya Ipuli,
S.L.P 310,

(46) _____
(47) _____

Katibu Mkuu,
Wizara ya Ujenzi,
(48) _____
Dar-es-Salaam.

(49) _____;

YAH: MAOMBI YA KAZI YA UFUNDI UJENZI

Husika na kichwa cha habari hapo juu. Mimi ni kijana mwenye umri wa miaka 22. Nimemaliza mafunzo ya ujenzi wa nyumba katika chuo cha VETA Mbeya mwaka, 2018 na kufaulu kwa daraja A. Naomba kazi ya ufundi ujenzi katika wizara yako. Naamini naweza kufanya kazi hiyo kwa ufanisi. Pamoja na barua hii nimeambatanisha vyeti vya Sekondari na chuo.

Ninatumiaini maombi yangu yatakubaliwa.

(50) _____

Enia Chakubanga

| |
|---|
| Wako mtiifu, Tabora, S.L.P 400, 28 -5-2019, Ndugu |
|---|